JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

Juni,2024

Dodoma

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS - TAMISEMI

Namba za Simu: 026-2321163

Mkuu wa Shule: 0784-531 333

Makamu Mkuu wa Shule: *0784-632 166 / 0784-571 189*

Matron: 0756-823 705

Shule ya Sekondari Dodoma

S.L.P 32

DODOMA

Tarehe Juni, 2024

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……………………………………………

S.L. P ……………………………………………

**Yah: MAELEKEZO VA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE VA SEKONDARI DODOMA HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA MKOA WA DODOMA MWAKA 2024.**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya ……………………
Shule ipo umbali wa kilometa nane kutoka kituo kikuu cha mabasi yaendayo mikoani (nane nane). Unaweza kufika shuleni kwa kutumia usafiri wa daladala na kushukia kituo cha sabasaba kwa nauli ya Tshs. 500/=. Shule ipo jirani kabisa na kituo cha daladala cha sabasaba na inapakana na Kituo cha Afya cha Makole upande wa magharibi, na Majengo ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania upande wa kusini mashariki.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 01 Julai 2024, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 30 Juni 2024. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 15 Julai 2024

2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni sketi ndefu inayofika kwenye vifundo vya miguu (ankle) ya rangi ya *dark blue* yenye marinda ya kupanga yenye upindo (belt) wa inchi mbili isiyo na mikanda.(inapatikana kwa Tshs. 27,000/= karibu na duka la shule kwa atakayependa)

ii. Shati jeupe mikono mifupi lililoshonewa namba tano ya kirumi V Kwenye mabega vote mawili (kwa kutumia kitambaa cha sketi) itakayosomeka kwa mbele lenye nembo ya shule. (linapatikana kwa Tshs.15,000/= karibu na duka la shule kwa atakayependa)

iii. Wanafunzi wanaovaa hijabu mashati yao ni mikono mirefu na hijabu nyeupe isiyo na urembo ya kuvaa sambamba na sare ya shule na sio vilemba au mitandio. Ni muhimu kuhakikisha hijabu inafunika kifua sambamba na viwiko viwili vya mikono akisimama. (inapatikana karibu na duka la shule kwa Tshs.12,000 kwa atakayependa)

iv. Viatu vya rangi nyeusi vya kufunga na kamba visivyo na visigino virefu pamoja na soksi ndefu nyeupe jozi mbili. Viatu vyenye kuacha sehemu ya miguu wazi vijulikanavyo simpo haviruhusiwi shuleni.

v. Sare ya Michezo ni *tracksuit* ya rangi ya dark blue yenye mistari myeupe ubavuni yenye lebo ya shule. (inapatika karibu na duka la shule kwa Tshs. 23,000/= kwa atayependa)

vi. Sweta la blue mtindo wa V shingoni lenye nembo ya shule;(linapatikana karibu na duka la shule kwa Tshs. 15,000 kwa atakayependa)

vii. Nguo za kushindia ni sketi ndefu ya rangi nyeusi inayofika kwenye vifundo vya miguu yenye pindo la inchi mbili zenye marinda ya kupanga na zisizo na mikanda. Wanaovaa hijabu watavaa hijabu nyeusi zenye kufunika kifua na viwiko viwili vya mikono;(zinapatikana karibu na duka la shule kwa Tshs. 27,000/= kwa atakayependa)

viii. Suruali 2 za kitambaa nyeusi isiyobana na jaketi la blue lisilo na urembo au maandishi litavaliwa usiku wakati wa kujisomea(preparation).(zinapatikana kwa Tshs 25,000/=karibu na duka kwa atakayependa)

ix. Tisheti (T-shirt) rangi ya Maruni na kijivu zenye nembo ya shule zitavaliwa baada ya vipindi vya darasani na siku za mwisho wa juma yaani Jumamosi na Jumapili(zinapatikana shule kwa Tshs. 15,000/= kwa atakayependa.

2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari Quire 4 kulingana na tahasusi aliyochaguliwa;

ii. Ream (A4) ya Karatasi nyeupe Mbili (2) kwa mwaka;

iii. Vitabu vya ziada vya masomo ya tahasusi husika;

iv. Dissecting Kit na Dissecting dish/tray kwa wanafunzi wanaosoma Biology;

v. Flash GB 4 na Head Phone kwa tahasusi ya PMC's;

vi. Scientific Calculator;

vii. Godoro la futi 2.5 kwa futi 6 kwa inchi 8 (2.5x 6 futi kwa 8 inchi); linakodishwa shule kwa Tshs 20,000/= kwa atakayependa.

viii. Shuka rangi ya blue Jozi 2, foronya ya bluu ya godoro 1, chandarua rangi nyeupe1;

ix. Taulo na Nguo za ndani za kutosha;

x. Vyombo vya chakula vya plastiki kontena lenye vyumba vitatu.

xi. Ndoo 1 kubwa (lita 20) yenye mfuniko (nyeupe) isipokuwa tahsusi (combination) ya EGM ambao watakuja na pasi moja ya mkaa;

xii. Sabuni ya maji ya chooni lita 5, **inapatikana shuleni.**

**N.B** Mzazi unakumbushwa kumpatia mwanao bima ya afya, nakala ya matokeo (result slip), Leaving certificate, na akaunti namba ya Benki ya mwanafunzi kwaajili ya matumizi yake awapo shuleni, kama hana akaunti namba ya benki aje na **NIDA** ya mzazi kwaajili ya kufungulia akaunti.

2.3 Michango mbalimbali

a) Shule za Bweni

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000 |
| 3 | Tahadhari | 5,000 |
| 4 | Nembo | 5,000 |
| 5 | Kitambulisho cha Shule | 5,000 |
| | Jumla | *80,000/* |

Muhimu: Michango yote ilipwe kupitia akaunti Namba **50501100160 DODOMA SECONDARY SCHOOL - RUZUKU** iliyopo NMB. Risiti zote za malipo (Bank pay in slip) ziwasilishwe Ofisi ya Mhasibu na kupatiwa risiti ya mfumo wa malipo serikalini. Epuka kulipa michango kwa fedha taslimu au kwa njia ya simu.

3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaii wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);

iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii;

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote;

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;

ix. Kutunza mali na miundombinu ya shule;

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

∴ Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

∴ Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

∴ Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;

ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila *taarifa/utoro;*

iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;

viii. Uvutaji wa sigara;

ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;

x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;

xi. Kusababisha mimba;

xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za *nchi;*

xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;

xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;

xv. Kudharau Bendera ya Taifa;

xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na

xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo. fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

.........................

FRANCIS W. TUMAINI

**MKUU WA SHULE**

DODOMA SECONDARY SCHOOL
THE HEADMASTER
P.O.BOX 32
DODOMA

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazl husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

>- Mkuu wa shule : 0784.531333

>- Makamu Mkuu wa Shule: 0784 - 571189

>- Mwalimu EK (sare ya shule, n.k): 0716 - 620702

>- Mwandamizi Malezi:0756 - 823705


IDADI VA MADAFTARI KWA KILA TAHASUSI
(Mwanafunzi anaweza kuwa na idadi Zaidi hii kulingana na uhitari wake binafsi)

| | TAHASUSI | IDADI VA MADAFTARI |
|---|---|---|
| 1. | HGL | 4 |
| 2. | HGK | 4 |
| 3. | EGM | 4 |
| 4. | CBG | 5 |
| 5. | PMC's | 4 |
| 6. | PCM | 4 |
| 7. | PCB | 5 |

## Zingatia Kielelezo cha sare za shule



Mfano wa sare sahihi



Mfano wa sare sahihi kwa Mwanafunzi wa kiislamu



Uvaaji wa masweta kipindi cha baridi



Aina ya malinda na sehemu sahihi ya kuvalia sketi

Mfano wa Viatu vya gidamu vilivyofunika miguu





Mfano wa bakuri sahihi ya chakula

# FOMU NA. 1: AHADI YA MZAZI / MLEZI

Mimi ............................................................wa S.L.P.................Mji. ..........................Simu Na.........................Ambaye kazi yangu ni ................................... natamka hapa kama mzazi / mlezi wa ..............................................Ninakubali kwa hiari yangu mwanangu asome katika shule ya Sekondari Dodoma kuanzia tarehe ..........................Ninaahidi kama ifuatavyo:-

1. Kwamba nimekubali chaguo alilopewa mwanangu na sitamruhusu kubadilisha hadi apate kibali cha maandishi kutoka kwa mamlaka husika.
2. Ninaahidi kumpatia mwanangu vifaa vyote kama vilivyoainishwa katika fomu ya kujiunga ikiwemo SARE KAMILI ya shule bila kuharibu chochote.
3. Ninatambua ya kuwa walimu wanahitaji ushirikiano wangu katika kumpatia mwanangu elimu na nitashirikiana nao bega kwa bega kwa maswala yanayomuhusu mwanangu kitaaluma na nidhamu ili aweze kufikia malengo yake na ya Taifa.
4. Naahidi kuwa endapo mwanangu ataenda kinyume na taratibu zilizoainishwa katika fomu hii achukuliwe hatua stahili za kinidhamu kama alivyoorodheshewa.

Jina.............................................saini...............tarehe..............Uhusiano na mwanafunzi..........

# FOMU NA. 2: AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi mwanafunzi ........................................................Wa kidato cha Tano chaguo ...................... (tahasusi) mwaka 2024 / 2025.Ninakiri kusoma, kuelewa na kuahidi kutii taratibu zote zilizoainishwa katila fomu iliyotumwa kwangu na Mkuu wa shule ya Sekondari Dodoma. Nitatoa ushirikiano wa kutosha kwa walimu wangu na shule kwa ujumla katika muda wangu wote nitakaokuwa shuleni ili niweze kupata elimu na kuendeleza jamii na taifa langu.

Jina............................................saini......................Tarehe.................

**Maoni ya Mkuu wa Shule**

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

# FOMU NA. 3: UTHIBITISHO WA MZAZI / MLEZI

Mimi.............................................wa.......................S.L.P. .......Mji............................ Simu Na.......................Nakiri kukaa na kuzungumza na mwanangu juu ya taratibu na sheria za shule na ninaahidi kumsaidia na kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Mkuu wa Shule na walimu kwa muda wote ambao mwanangu atakapokuwa katika shule hii. Ninatambua madhara ya mwanangu kutembelewa na wageni wasioeleweka wakati akiwa shuleni na ninaomba shule iwatambue watu wanne(4) ambao wanahusika katika muda wote ambao atakuwa shuleni nao ni:- (ambatanisha picha passport size zao)

1. Jina.........................................................................................

   Simu............................................ uhusiano.....................

2. Jina .........................................................................................

   Simu............................................ uhusiano...................

3. Jina.........................................................................................

   Simu............................................ uhusiano...................

4. Jina .........................................................................................

   Simu........................................ uhusiano..................

Saini ya mzazi / mlezi...................................Simu...........................Tarehe:.........................

# FOMU NA. 4: UTHIBITISHO WA AFYA

Dodoma Secondary school
P.O. BOX 32
DODOMA.

## MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by Medical Officer from a known Public Hospital or Health Centre in respect to all entrants

Full name ..........................................................Age.........Sex...........year..............

1. Blcod count (Red and White) ...........................................................
2. Urine analysis Test ...........................................................................
3. Syphilis test .....................................................................................
4. T.B. ....................................................................................................
5. Eye Test ............................................................................................
6. Ears ...................................................................................................
7. Spleen ...............................................................................................
8. Abdomen ...........................................................................................

ADDITIONAL INFORMATION: e.g. Physical impairment, family disease, chronic infections etc.

..........................................................................................................................
..........................................................................................................................
..........................................................................................................................

I certify that the above named individual is fit to pursue studies as stated above

.....................................
Name and Designation

...........................................
Signature and Official stamp

.........................................
STATION

...................................
DATE

**NOTE:**

1. Medical officer during the course of this Examination please attend the individual according to any diagnosed case.
2. The dully filled form must be handed to the Head of the School during registration week, under No circumstances should a student be registered without certification of his/her physical fitness.